**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**Simu namba 0784997190 au 0767357649 Shule ya sekondari Hai,**

**S.L.P 217 HAI**

**Ndugu______________________________________**

**TAREHE_____________________________**

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE KIDATO CHA TANO MWAKA 2020/2021:**

**1.0** Nafurahi kukujulisha kuwa umechaguliwa /Umekubaliwa kuhamia/kujiunga katika shule hii kama mwanafunzi wa kidato cha tano, Chaguo la PCM- PCB- PGM-

**2.0** Shule ya sekondari Hai iko kilomita tatu (3) kutoka stendi ya mabasi Bomang'ombe, kando ya Barabara kuu ya Moshi - Arusha.

**3.0** Shule itafunguliwa tarehe **_____________** wanafunzi wote wanatarajiwa kuwasili shuleni siku hiyo yakufungua shule kuanzia saa 8:30 mchana.

**4.0** Wanafunzi watakaotimiza maagizo yote ya kujiunga na shule ndio watakaokubaliwa kuandikishwa na kuendelea na masomo.

**5.0** Kama umekubali nafasi hii tekeleza maagizo yaliyoorodheshwa, na jaza fomu A,B na C. na kurudisha shuleni siku utakapowasili.

**6.0 ADA NA MAHITAJI MENGINE YA SHULE:**

**6.1 ORODHA KUU YA FEDHA ZINAZOHITAJIKA ILI MWANAFUNZI APOKELEWE SHULENI:**

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Ada ya mwaka | 70,000/= |
| 2. | Fedha ya tahadhari | 5000/= |
| 3. | Kuboresha taaluma | 20,000/= |
| 4. | Kitambulisho | 5000/= |
| 5. | Fedha ya matibabu | 10,000/= kwa asiye na bima ya afya |

| | | |
|---|---|---|
| 6. | Fedha ya kukodi Godoro | 10,000/= kwa anaehitaji |
| 7. | Mchango wa walinzi , wapishi na wahudumu | 30,000/- |
| 8. | Ukarabati | 15,000/= |
| 9. | Nembo | 2000/= |
| | **Jumla kuu** | **167,000/=** |

Fedha za Ada zilipwe Banki Akaunti namba 4011200086. Jina la Akaunti ni Hai Sec School Recurent A/C. Fedha za michango ya shule zilipwe Akaunti Na 4013500122 Jina la Akaunti ni Hai sec school Self. Reliance A/C – A/C zote ni NMB.

**UJE NA PAY-IN-SLIP KWA UTHIBITISHO ILI UPEWE RISITI SHULENI: FEDHA TASLIMU HAZIPOKELEWI SHULENI:**

**6.2 SARE YA SHULE**

1. Suruali Mbili (2) za rangi ya **ugoro**
2. Mashati mawili meupe ya mikono mifupi Mwanafunzi aje nayo na **TAI** yenye rangi ya suruali
3. Viatu vya ngozi nyeusi vyenye kamba na visivyo na visigino virefu wala mapambo.
4. Soksi za rangi ya ugoro jozi mbili.

**6.3 SARE BAADA YA MASOMO**

I. Suruali nyeusi Mbili, zisizobana, Zitakazovaliwa siku ya Jumamosi na Jumapili na

Baada ya masomo.Haturuhusu kuvaa Nguo Zingine tofauti na hizo

Hairuhusiwi kuja na Sweta , Jacketi au Koti la aina yeyote.

II. Raba/ Viatu vya michezo.

III. Bukta ya rangi ya blue kwa ajili ya michezo.

IV. Truck suit moja rangi ya light blue.

**6.4 VIFAA VYA BWENI**

1. Blanketi moja.
2. Shuka mbili za rangi ya blue.
3. Bedcover moja ya blue isiyo na urembo wa aina yeyete.
4. Mto na foronya ya blue.

5. Chandarua (Mosquito Net).

6. Taulo, Mswaki , Sabuni, Malapa nk.

7. Sanduku MOJA na Begi dogo jeusi lakubebea vitabu vya darasani.

**VIFAA VYA CHAKULA:**

Sahani, Bakuli, Kijiko, na Kikombe cha Udongo.

**6.5 VIFAA VYA MASOMO:**

1. Madaftari Makubwa Counter Books
2. Mathematical Sets na Scientific Calculator.
3. Kalamu za kutosha Rular Penseli nk.
4. Vitabu vya Rejea kulingana na masomo (Mchepuo) kwakuwa vitabu vilivyopo havitoshelezi kwa kila mwanafunzi. Aidha orodha ya vitabu hivyo Imeambatanishwa na fomu hii.
5. Wanafunzi waje na vitabu vya ibada kulingana na madhehebu yao.
6. Picha 4 Pasportsize
7. Ream moja ya karatasi nyeupe zisizo na mistari- size $A_4$

**6.8 VIFAA VYA USAFI**

| PCM | PCB | PGM |
|---|---|---|
| **Water squizer,slasher,ndoo ndogo moja** | **Slasher,mopper,ndoo moja** | **Hadbroom,softbroom na ndoo ndogo moja** |

**6.9 VIFAA AMBAVYO MWANAFUNZI HARUHUSIWI KUJA NAVYO:**

Nimarufuku kwa mwanafunzi kuja na vitu vifuatavyo.

1. Simu za mikononi
2. Pasi ya Umeme
3. Heater
4. Redio/ Redio cassette
5. Kamera
6. Vyakula vya aina yeyote
7. Vileo vya aina yeyote.

Mwanafunzi atakayepatikana na vifaa hivi ataadhibiwa na vifaa vitachukuliwa na havitarudishwa.

7.0 Sheria/ Kanuni/ Taratibu za shule lazima zifuatwe na zimeambatishwa na fomu ya kujiunga ( Joining Instruction).

## SHERIA ZA SHULE:

Sheria zote za shule zimewekwa walengwa / wanafunzi kulifika lengo lao la kuwepo hapa shuleni.

**1.** Kuwa mwanafunzi unapaswa **KUJITAMBUA** kuwa wakati uwapo mwanafunzi wa shule ya **Hai Sekondari** unaishi ndani ya utaratibu wa kiuanafunzi ndani na nje ya shule, usiku na mchana.

**2.** Kuongeza muda wa **RUHUSA HALALI** mfano kwenda hospitali, posta, n.k. ni kosa litakalosababisha mwanafunzi kupewa adhabu kali.
**3.** Mwanafunzi haruhusiwi kuchelewa kurudi shuleni wakati wa likizo.Anapochelewa afike shuleni na Mzazi/ Mlezi aliyeandikishwa shuleni akiwa na barua iliyopitishwa na **MRATIBU KATA** anapotoka, la sivyo atarudishwa Nyumbani.

**4.** Kutii viongozi ni wajibu wakila mwanafunzi. Wanafunzi wawaheshimu na kuwatii **WAALIMU WOTE NA WAFANYAKAZI WASIO WAALIMU,WAGENI** WOTE,wanaotembelea shule, viongozi wote na Taifa na Umma na Viongozi Wanafunzi.

**5.** Wageni wa aina yeyote hawaruhusiwi kufika /kupitia eneo la mabweni.Mwanafunzi haruhusiwi kuongea na mtu yeyote asiyekuwa mwanajumuiya wa shule hii katika eneo lolote la shule.

**6.** Ni marufuku mwanafunzi kuwa nje ya eneo analohitajika kuwepo.Ni lazima awahi na kushiriki katika shughuli zote za shule mfano kuitika mara moja na kukimbia na kuelekea mahali atakiwapo wakati anaposikia kengele au mwito mwingine , shughuli za uzalishaji mali, roll-call, usafi wa mazingira, michezo, kinyume na hapo utaadhibiwa vikali.

**7.** Ni marufuku na kosa kubwa sana kwa mwanafunzi kuendesha au kushiriki katika vyama ambavyo havitambuliwi na Uongozi wa shule. Haruhusiwi kuchezea vilabu vya michezo nje ya shule.

**8.** Nywele fupi zisizozidi urefu wa robo nchi na daima ziwe zimechanwa ndizo zinazoruhusiwa. Mwanafunzi yeyote haruhusiwi kunyoa kipara, panki/ Kisahani/Kiduku au kuweka dawa ya aina yeyote. Adhabu itatolewa kwa yeyote atakayekiuka.

**9.** Ruhusa kutoka nje ya shule hutolewa na Mkuu wa Shule au na Mwalimu mwingine kwa idhini ya Mkuu wa Shule. Kibali kiwe na saini pamoja na mhuri wa shule.Kibali cha kuhudhuria Msiba kitolewe kwa mwanafunzi aliyefiwa na Baba au Mama,(wazazi halisi wa wanafunzi) Dada au Kaka wa kuzaliwa tumbo moja. Hakuna ruhusa itakayotolewa kwa jamaa wengine zaidi ya hao.

**10.** Wakati mwanafunzi awapo nje ya shule kwa ruhusa ni lazima awe amevaa sare ya shule ,pia anapokwenda likizo na wakati wa kurudi.

**11.** Mzazi au mlezi aliyeandikishwa shuleni ndiye anayeruhusiwa kumwombea mwanafunzi ruhusa itakapolazimu hivyo na si vinginevyo.

**12.** Haruhusiwi mwanafunzi kuvaa nguo za nyumbani mbali na Nguo alizopewa shuleni.

**13.**Wanafunzi hawaruhusiwi kulala wawili kitanda kimoja kwa sababu zisizo za msingi wakikamatwa wataadhibiwa.

**14**. Hairuhusiwi mwanafunzi kuhama domu au chumba alichopangiwa adhabu kali itachukuliwa.

**MAKOSA MAKUBWA YANAYOWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE.**

1. Wizi
2. Uasherati na Ushoga
3. Ulevi wa aina yoyote na matumizi ya madawa ya kulevya
4. Kuanzisha kuchochea au kushiriki mgomo au fujo shuleni
5. Kuharibu kwa makusudi mali ya shule, walimu au watu wengine
6. Kutoheshimu Bendera ya Taifa, alama au fedha ya Taifa
7. Kusababisha mimba ndani na nje ya shule
8. Kuoa au kuolewa
9. Kutohudhuria shuleni kwa muda mrefu
10. Kukataa adhabu ya Mkuu wa shule
11. Kupigana na mwalimu, Mfanyakazi ,au Mwanafunzi.
12. Kukutwa na simu ya mkononi, Redio, CD n.k

**FOMU A:** **KIAMBATANISHO I**

# HATI YA MAKUBALIANO

**MKUU WA SHULE,**

**SHULE YA SEKONDARI HAI,**

**S.L.P.217,**

**HAI .**

## KUKUBALI NA KUFUATA SHERIA NA MASHARTI YA SHULE:

Mimi………………………………..nakubali nafasi ya kidato cha ……………………niliyopewa katika shule yako. Nakubali masharti na kuwa nitatii sheria za shule hizo nazile zitakazotolewa kwa muda wote wa masomo yangu. Naahidi kuwa nitawaheshimu na kuwatii walimu wa shule na wafanyakazi kama wazazi wangu.

Naahidi kuwa nitatii wale wote watakaoteuliwa au kuchaguliwa kuwa viongozi wangu kwa mujibu wa sheria.

Naahidi kuwa mwanafunzi mwaminifu. Naahidi pia kuwa nitajielimisha kwa nduvu zangu na akili zangu zote kwa manufaa yangu binafsi na Taifa langu.

Natambua kuwa nikikiuka ahadi nitapoteza nafasi yangu hapa shule.

JINA LA MWANAFUNZI…………………………………………..
SAHIHI………………………

JINA LA MZAZI/MLEZI……………………………………………..
SAHII………………………..

MZAZI/ MLEZI/ MWANAFUNZI:

Anwani ya Mzazi/Mlezi………………………………………………………………………

SIMU NA……………………………………………………….

e.mail:……………………………………………………………………..

Namba ya kuandakishwa:……………………………………………..
Tarehe……………………….

**FOMU:B** **KIAMBATANISHO II**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA HAI**

**SHULE YASEKONDARI HAI,**

**S.L.P.217, HAI.**

**SIMU NA 0784997190 / 0759123116**
**TAREHE:……………………..**

**MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI**

**JAZA FOMU HII KWA UKWELI HII NI SIRI YAKO NA MKUU WA SHULE TU:**

1. Andika majina kamili.
   i. Majina ya shule………………………………………………………
   ii. Majina ya nyumbani…………………………………………………..

| | **JINA** | **BABA** | **UKOO** | **UMRI** | **TAREHE YA KUZALIWA** |
|---|---|---|---|---|---|
| LAKO | | | | | |
| LABABA/MLEZI | | | | | |
| LA MAMA | | | | | |

2. **NYUMBANI:**
   Kijiji/Mtaa…………………………………kata………………………………..
   Taarifa…………………………………………………Wilaya……………………….
   Mkoa…………………
3. Anwani ya nyumbani…………………………Simu……………………………………
4. Kukiwa na matatizo taarifa ipelekwe kwa nani…………………………………
   Uhusiano na wewe?.....................................................................
5. Wazazi na Ndugu:
   Baba yuko hai?..........................................................Mama yuko hai?.............................................
   Baba ana watoto wangapi? ....................... Wavulana………… Wasichana…………
   Baba ana wake wangapi?.........................Wewe ni mtoto wake wangapi?.................
   Mko wangapi kwa mama huyo? Wewe ni mtoto wa ngapi kwa mama………
   Dini yako…………………………Madhehebu…………………………………

**UNAOWATEGEMEA:**

a) Unaishi na nani na wapi? ……………….. Simu yake……………..

b) Nani anayekupa mahitaji ya shule……………………………….Simu yake

SAHIHI………………………

TOA SABABU KAMA SIYO

MZAZI…………………………………………………………………

Shule ulizosoma:

a) Unaishi na nani na wapi?.........................................................Simu yake…………………

b) Nani anayekupa mahitaji ya shule…………………………….Simu yake………………….

SAIHI…………………………………………………………………………………………………………

TOA SABABU KAMA SIYO

MZAZI……………………………………………………………

Shule ulizosoma:

a) Shule ya msingi……………………………… Mwaka…………….. Hadi…………

b) Shule ya / za sekondari………………….Mwaka……………..Hadi……………

Majina ya watu 3 watakaohusika kuwasiliana na uongozi wa shule endapo utahitaji kwa suala lolote lile.

| JINA | ANWANI | SIMU | UHUSIANO | MAHALI ANAPOISHI |
|---|---|---|---|---|
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |

**MWISHO**

Nakutakia maandalizi mema na safari njema ya kuja kuanza masomo rasmi ya kidato cha tano shuleni Hai Sekondari.

Karibu sana

_________________

**MWL. Alex Warioba**
**Mkuu wa shule**